KAMATI YA BUNGE YATEMBELEA TUME

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, inayaoongozwa na Mbunge wa Kahama, Mh. James Lembeli imefanya ziara Tume ya Taifa ya Mipnago ya Matumizi ya Ardhi kukagua utekelezaji wa shughuli za mbalimbali za Tume tarehe 29/03/2011.

Akiikaribisha Kamati hiyo, Makamu Mwenyekiti wa Tume, Dr. Maria Mashingo, aliwataka wajumbe wa Kamati hiyo, wapokee taarifa ya utekelezaji wa kazi za Tume toka kuundwa kwake hadi sasa kwa kuzingatia dira yake ya kuwa Taasisi yenye uwezo na rasilimali kuongoza na kuwezesha mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi kwa maendeleo endelevu.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume Bw. Gerald Mango aliwaeleza Wabunge kuwa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ilianzishwa kwa Sheria Namba 3 ya Mwaka 1984 ambayo imekoma Mwezi Aprili 2007 baada ya kutungwa kwa Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Namba 6 ya Mwaka 2007.

“Majukumu ya msingi ya Tume ni kuratibu utayarishaji na utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi nchini ikiwa ni kusaidia na kuwezesha mamlaka za wilaya na vijiji kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi,” alisema Bw. Mango na kuongeza kuwa, “Tume imekuwepo, ili kuendeleza taaluma ya kupanga matumizi ya ardhi, kuhamasisha umma kushiriki katika mipango ya matumizi ya ardhi, pamoja na kusimamia utekelezaji wa mipango iliyoidhinishwa.”

Akielezea utekelezaji wa kazi za Tume, Mkurugenzi Mkuu aliiambia Kamati kuwa, Tume imefanikiwa kuandaa Mpango wa Taifa wa Matumizi ya Ardhi ambao utakuwa ni dira ya Taifa ya jinsi ya kuitumia ardhi yote ya Tanzania Bara kwa manufaa na maendeleo ya uchumi na jamii ya nchi hii na kwa ustawi wa kila mtumiaji ardhi. Mpango huo una nia ya kuweka viwango vya mgawanyo wa ardhi, kuainisha matumizi makuu ya ardhi na kuondoa migongano ya sera mbalimbali juu ya matumizi ya ardhi.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume Bw. Gerald Mango (aliyesimama) akiileza Kamati ya Bunge juu ya utekelezaji wa shughuli za Tume. Katikati ni Mwenyekiti wa Kamati, Mh. James Lembeli na kushoto ni Makamu Mwenyekiti, Mh. Abdulkarim Shaha.

Vilevile, hapo kabla, Tume imeweza kuandaa mipango ya Kanda kutambua maeneo ya uwekezaji wa nje na ndani. Aidha, mipango hii hutambua maeneo ya Kilimo, ufugaji, misitu na nyuki, madini, vyanzo vya maji na makazi ya binadamu. Mipango ya kanda ni muhimu Kitaifa kwani inaonyesha rasilimali za Taifa, mgawanyo wake na uwezo wake kwa kuzalisha na kutegemeza maisha ya binadamu na viumbe mbalimbali.

Pamoja na mipango hiyo, Tume pia imefanikiwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya Wilaya na Vijiji sehemu mbalimbali hapa nchini. Mipango ya Wilaya ni mhimili wa uendelezaji wa matumizi bora ya ardhi wilayani; kitalaamu na kuwa na taarifa na takwimu mbalimbali za ardhi na rasilimali zake wilayani. Mipango hii ni hadidu za rejea ya msingi katika kufanya maamuzi juu ya matumizi bora ya ardhi wilayani. Mipango hii huainisha maeneo ya Ardhi ya Hifadhi, Kawaida na Vijiji ambayo husimamiwa na wadau tofauti kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya 1999.

Mkurugenzi Mkuu aliiambia kamati kuwa Tume imefanikiwa kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji kwa kuzingatia kuwa ni zana muhimu kwa usimamizi wa rasilimali hii na kwa maendeleo endelevu. Wanavijiji na taasisi zao wanahitaji kujenga taratibu, uwezo wa kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi yao kwa kutilia maanani kuwa Watanzania walio wengi wanaishi vijijini na ardhi ndiyo mtaji mkuu wanaoutegemea. Katika uchumi unaotegemea kilimo na ufugaji, uvuvi, na uvunaji wa mazao ya misitu, mipango ya vijiji itawafanya Watanzania waweze kuishi maisha bora bila kuwa tegemezi wa misaada ya nje kama wataitumia ardhi yao vizuri.

Akipokea taarifa hiyo, Mwenyekiti wa Kamati, Mh. James Lembeli (MB) aliipongeza Tume kwa kazi nzuri iliyofanyika na kukiri kutambua changamoto inayoikabili hasa ufinyu wa bajeti inayofanya kazi za mipango ya matumizi ya ardhi kuwa na kasi ndogo. Wajumbe wa kamati waliitaka Tume kuhakikisha inafika nchi nzima na kutoa elimu kwa umma juu ya mipango ya matumizi ya ardhi. Aidha, wajumbe waliahidi kuisimamia Tume na kuhakikisha inapata bajeti itakayotosheleza kufanya kazi zake pamoja na kuishauri Serikali kuweka mipango ya matumizi ya ardhi kama kipaumbele cha Taifa, kwani bila ardhi kupangwa mambo hayaendi.

Mbali na kutembelea makao makuu ya Tume, Kamati hiyo pia ilifanya ziara katika masjala ya ardhi ya Wilaya ya Kisarawe na kijiji cha Mitengwe kilichopo Wilayani humo kujionea utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi pamoja na ufunguzi rasmi wa ofisi ya masjala ya ardhi ya kijiji hicho.

Wakiwa kijijini Mitengwe, wajumbe wa Kamati walipata fursa ya kusikia taarifa ya jinsi utekelezaji wa mpango wa matumizi ya ardhi ulivyofanyika kijinini hapo, kuanzia hatua ya kwanza ya kutoa elimu kwa halmashauri ya kijiji na mkutano mkuu wa kijiji hadi kwenye ujengaji wa masjala ya ardhi kwa ajili ya kuhifadhia hati miliki za kimila.

Akifungua masjala ya Ardhi ya kijiji Mh. Lembeli aliwapongeza wananchi wa Mitengwe na kuwataka kuitunza masjala hiyo, kwa ajili ya vizazi vya sasa na vya baadae. Mh. Lembeli pia aliahidi kuwapeleka Madiwani wa Kahama kijijini Mitengwe ili nao wajifunze juu ya mipango ya matumizi ya ardhi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Mh. James Lembeli (Kulia) akifungua rasmi Masjala ya Ardhi ya Kijiji cha Mitengwe. Kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Mh. Halifa Karamagi